East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 2, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Kubainisha Usawiri wa Ukahaba naWahusika Makahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi

*Karuhanga Deusdedit*[1*]*, Prof. Florence Indede, PhD*[1] *& Dkt. Deborah Nanyama Amukowa, PhD*[1]

[1] Chuo Kikuu cha Maseno, S. L. P. 3275-40100, Kisumu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: karuhangad1@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*23 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Ukahaba, Ngono, Kuwadi, Madanguro.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema (Mohamed S.Mohamed) na Ndoto ya Almasi (KenWalibora).* Kitendo cha ukahaba kimesababisha mashaka mengi sana katika maisha ya mwanadamu kama vile kupoteza ujira, uharibikaji wa ndoa maradhi ya zinaa, vifo, kukata tamaa na utengano miongoni mwa wanajamii. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni: kubainisha usawiri wa ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*; Mtafiti alitumia nadharia ya utekelezi ambayo ni miongoni mwa nadharia nyingi zenye mtazamo wa kisosholojia. Nadharia ya utekelezi imeendelezwa na wanasosholojia kama vile TalcortParsons na EmileDurkheim kama wanavyonukuliwa na Worsely*IntroductiontoSociology* (1970), huku akisema kwamba ukahaba husababishwa na mambo mawili yaani haja ya kutekeleza mahitaji ya kiuchumi na kwa kukidhi matashi ya nafsi zao kiashki. Mtafiti pia alitumia nadharia ya umaksi iliyoanzishwa na Karl Marx (1818-1863) na FredrichEngles(1820-1895). Nadharia hii hufaa utafiti huu kwa kudhihirisha wahusika wanaoshiriki katika vitendo vya ukahaba kwa ajili ya kupata fedha au zawadi. Mabepari au walionacho huwa na lengo la kuridhisha miili yao tu na wanyonge huwa na lengo la kupata pesa ili kutimiza mahitaji yao, pengine, mnyonge hutolea mwili wake kwa ajili ya kupewa kazi au kupandishwa cheo kazini au kama njia ya kuilinda kazi yake ili asipigwe kalamu. Utafiti huu ni wa maktabani kwa hivyo, maktaba yaliyotumika ni yale ya Chuo Kikuu cha uislamu kilichopo nchini Uganda, Chuo kikuu cha Kimataifa Metropolitan, na maktabani ya shule ya upili Heritage. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na uchunguzaji wa riwaya teule yaani: ile ya *Nyota ya Rehema* na ya *Ndoto ya Almasi* kwa kuzisoma na kuzichambua kwa kina na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

kuiwasilishwa data kwa mbinu ya kiuthamano. Utafiti huu umebainisha kuwa wahusika hufanya ukahaba ili kupata pesa au kuridhisha matashi ya nafsi zao kiashiki. Utafiti huu utakuwa wa muhimu sana kwa kufunza jamii kwamba kahaba si mwanamke peke yake kama inavyochukuliwa katika baadhi ya jamii bali kahaba ni mtu yeyote awe mwanamume au mwanamke anayeshiririki vitendo vya uzinzi.

**APA CITATION**

Deusdedit, K., Indede, I. & Amukowa, D. N. (2022). Kubainisha Usawiri wa Ukahaba naWahusika Makahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 155-173. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005.

**CHICAGO CITATION**

Deusdedit, Karuhanga, Florence Indede and Deborah Nanyama Amukowa. 2022. "Kubainisha Usawiri wa Ukahaba naWahusika Makahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 155-173. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005.

**HARVARD CITATION**

Deusdedit, K., Indede, I. & Amukowa, D. N. (2022) "Kubainisha Usawiri wa Ukahaba naWahusika Makahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 155-173. doi: 10.37284/jammk.5.2.1005.

**IEEE CITATION**

K. Deusdedit, I. Indede & D. N. Amukowa "Kubainisha Usawiri wa Ukahaba naWahusika Makahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 155-173, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Deusdedit, Karuhanga, Florence Indede & Deborah Nanyama Amukowa. "Kubainisha Usawiri wa Ukahaba naWahusika Makahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 155-173, doi:10.37284/jammk.5.2.1005.

## UTANGULIZI

Kitendo cha ukahaba chaweza kufasiliwa kama mwenendo wa mwanaume na mwanamke kushiriki katika kitendo cha ngono kama biashara au kwa kukidhi matashi, ukahaba, uasherati, uzinifu na uzinzi (TUKI, 2004). Riwaya nyingi za Kiswahili zilizoandikwa baada ya uhuru na kuendelea hadi hii leo zinalenga kujenga jamii mpya kwa kuielimisha, kuikosoa, kuionya na kwa kiasi fulani kuiburudisha(Nguma, 2001).

Kulingana na Mbilinyi (1983:14-16), mwanamke alikuwa akichukuliwa kama chanzo cha utafiti barani Afrika kuanzia miaka ya sitini na sabini kipindi cha kupigania uhuru kwa nchi nyingi za Afrika. Nyanja mbalimbali za serikali zilihamasishwa kuanza utafiti kuhusu mwanamke, idadi kubwa ya wanawake iliyokuwa ikijihusisha na ukahaba, wasichana wengi kupata mimba, na wengine kukimbilia mjini kisha ukahaba ukaongezeka miongoni mwa wanawake na wasichana katika vichochoro vya miji.

Bakwesigha (1982:11), anasema kwamba, ukahaba lina uhusiano mkubwa na unyonge, unyonge katika muktadha huu unamaanisha udhaifu wa nafsi na udhaifu wa elimu. Ilhali, ukahaba ni uhitaji wa kifedha na kukidhi matashi ya nafsi (mapenzi yasiyojali ndoa). Kuna unyonge unaosababishwa na kupoteza au kutengwa na walezi, hali hii huleta fedheha kwa taswira ya malezi mabaya ambapo talaka nyingi hutokea, ndoa huvunjika na mara nyingi husababisha unyonge wa nafsi na kiuchumi. Kwa hiyo, kazi hii iliangazia jinsi unyonge unavyowalemaza wahusika wengi mpaka wakajiingiza katika vitendo vya ukahaba. Katika mantiki hii, kuna swali, je! Mwanamke ndiye kahaba peke yake au mwanamume pia ni kahaba? Wataalam mbalimbali wametoa suluhisho la swali hili kama vile; Waniston Dictionary (1948), hufasiri kahaba kama; mwanamke au mwanamke anayeshiriki mambo ya uzinifu au uzinzi au uasherati kwa lengo la kupata fedha.

Kishtainy na wenzake (1982:32) wanaeleza kuwa, kahaba ni mwanamke au mwanamme anayeshiriki

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

mapenzi ya watu wengi kwa matarajio ya pesa au zawadi bila kuwa na hisia za mapenzi ya dhati, pia wengine hufanya ukahaba kwa ajili ya kuridhisha nafsi zao kiashiki. Katika muktadha huu, ni muhimu tubainishe mambo yanayomtambulisha kahaba, kuna uthibitisho kwamba kahaba awe wa kike au wa kiume, daima hutolea mwili wake kwa ajii ya mapato au Kitu kingine.

**Nadhariaza Utafiti**

TUKI (2004), wanafasili nadharia kuwa ni dira, mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kufafanua, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Nao, Wafula na Njogu (2007), wanaeleza kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza mtu wakati wa kusoma kazi ya fasihi na kuifahamu katika vipengele vyake vyote. Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kwamba nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyoibuka kutokana na majaribio ya jambo hilo. Mdee na wenzake (2011), wanaeleza kuwa nadharia ni mpango wa mawazo yaliotungwa ili kuongoza na kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Jilala (2016), anaifasili nadharia kuwa ni wazo ambalo huzuka kama dira kwa msomaji ama mchambuzi na hali mwanafasihi alivyolinganisha katika kutoa majumulisho ya kazi za fasihi na zisizo za fasihi. Kutokana na fasili hizo tunaweza kusema kwamba nadharia ni kigezo kinachotumika kumwelekeza mtu katika kuchunguza au kutathmini jambo fulani. Kwa kuwa ukahaba ni suala lenye mawanda rnapana sana, nadharia moja haitoshi kulitatathmini bali mtafiti aliona heri kutumia nadharia mbili yaani nadharia ya umaksi na ya utekelezi ili kulitathmini kiukamilifu. Hii ni kwa sababu ukahaba husababishwa na hali mbalimbali za kiuchumi, kisaikolojia na kisosiolojia.

**Nadharia ya Umaksi**

Nadharia hii ilianzishwa na Karl Marx (1818-1863) na FredrichEngles (1820-1895), katika nadharia hii, Marx amejikita katika historia na miundo ya kijamii kwa kupitia hoja kuu tatu zifuatazo: Historia ya maisha ya mwanadamu yaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo inachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi pia huathiri uzalishaji mali na usambazaji wa mali hizo. Hivi vyote kwa pamoja huunda misingi ambapo kwenye misingi hiyo huunda maadili, itikadi, dini na utamaduni. Hoja nyingine ni kuamini kuwa historia ya binadamu inadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi jamii. Marx alisema “Historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka katika jamii” Nadharia ya Kimaksi inaangalia matabaka katika ngazi mbalimbali kama vile ngazi ya familia, dini na elimu. Ubepari kama njia ya uzalishaji mali na mara nyingi huathiriwa na tabaka la chini hivyo ubepari hujitengenezea njia za kujiharibu wenyewe kutokana na unyonyaji na ukandamizaji unaotendeka kwa tabaka la chini. Mabepari hawa au walionacho kulingana na Marx ni tabaka la wale ambao wana uwezo wa kununua nguvu za wengine na wenye mali wakazalisha mali zaidi. Anaendelea kusema kuwa wasionacho ni lile kundi la watu ambao huuza nguvu zao kwa mamwinyi na kipato wanachokipata mara nyingi huwa hakiwatoshi.

Matabaka mbalimbali husababishwa na mali, siyo kipato tu. Marx huendelea kusema kuwa walionacho huendelea kuwanyonya wasionacho na kuwalipa kipato kinachotosha kununua chakula na kulipia makazi yao, na wafanyakazi wanaoshindwa kuelewa kuwa wananyonywa huchukulia kusema kuwa wao wako afadhali. Nadharia hii hufaa utafiti huu kwa kudhihirisha wahusika wanaoshiriki katika vitendo vya ukahaba kwa lengo la kupata fedha au zawadi. Mabepari au walionacho huwa na lengo la kuridhisha matashi ya nafsi zao kiashki na wanyonge huwa na lengo la kupata pesa ili kutimiza mahitaji yao, pengine, mnyonge hutolea mwili wake kwa lengo la kupewa kazi au kupandishwa cheo kazini au kama njia ya kuilinda kazi yake ili asipoteze ujira. Hapa tunavumbua kwamba tabaka la chini katika jamii hukandamizwa na tabaka la juu kwa kuwa mnyonge huwa anataka kupata riziki na kwa hiyo hana hiari yoyote bali kumtegemea bepari maana ndiye mwenye jibu la mashaka yake kwake. Kulingana na msimamo wa nadharia hii, wanadamu katika jamii hushiriki na kujiunga na taasisi za ukahaba sio kwa hiari yao bali kwa madhumuni ya kupata fedha ili waepukane na hadhi ya unyonge lakini wanachopewa huwa hakitoshi na kwa hiyo huendeleza shughuli za ukahaba kama kazi yao rasmi ya kuwapa riziki. Nadhari ya umaksihaijitosherezi peke yake kwa hivyo nadharia ya utekelezi ilitumika pia ili kuelezea suala la wahusika kufanya ukahana ili kukidhi miili yao.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

### Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* (Mohamed S.Mohamed) na *Ndoto ya Almasi* (KenWalibora).

## MBINU ZA UTAFITI

Sura hii inahusu mbinu za utafiti ambapo inabainisha na kueleza mbinu zilizotumika katika mchakato wa utafiti huu. Mtafiti alianza kwa kubainisha eneo la utafiti, utaratibu wa utafiti, njia za ukusanyaji wa data, sampuli na mbinu za uteuzi wa sampuli, vifaa vya kukusanyia data na uchambuzi wa data.

### Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kiuthamano, ulitumia mbinu ya usomaji makini na uchunguzaji wa riwaya teule yaani: riwaya ya *Nyota ya Rehema* na riwaya ya *Ndoto ya Almasi*. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kuzihakiki riwaya hizi mbili kwa kutumia na kuongozwa na msingi wa Nadharia ya utekelezi na umaksi.

### Uteuzi wa Sampuli

Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi fulani cha vitu au watu kilichomo ndani ya mkusanyiko wa watu ambacho mtafiti anaamini kwamba kikundi hicho kitampatia taarifa anayohitaji kuhusu utafiti wake. Kwa sababu hiyo, mtafiti hulazimika kuteua kitu fulani au watu ambao huitwa kundi lengwa. Kwa hiyo katika utafiti huu, mtafiti alitumia riwaya ya *Nyota ya Rehema na* riwaya ya *Ndoto ya Almasi* kwa sababu riwaya hizi zimebeba uwanja wa vipengele vya ukahaba ambavyo mtafiti alikusudia kuvichunguza kwa kina kwa kuangalizia wahusika wanaoshughulika na vitendo vya ukahaba, sababu zinazowaletea kufanya ukahaba na athari zinazowapata.

### Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Scale (2012) na silver (2010), wanasema kwamba zipo mbinu mbalimbali za kukusanya data na katika mbinu hizo hakuna mbinu inayojitosheleza katika mazingira yake. Mbinu ya usomaji matini kwa kusoma kitabu teule riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* zilitumiwa. Data ilikusanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Pia tasnifu zenye uhusiano na mada ya mtafiti zilisomwa kwa makini.

### Mbinu ya Maktaba

Kothari (2004) anaelezea mbinu hii kuwa ni mbinu inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, tahakiki, magazeti, majarida, na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti ili kupata data zilizokidhi haja ya kiutafiti pamoja na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba inafahamika kuwa tafsiri huwa katika matini mbili zilizoandikwa (rej. Cartford, 1965; Newmark, 1981 na Mwansoko 1996). Nao Pyne&Weber (2007) wanasema kuwa matini hutoa taarifa za awali. Kwa maana hiyo, matini andishi ndiyo chanzo kikuu cha data ya tafsiri. Katika utafiti huu matini andishi ndiyo ilikuwa chanzo kikuu cha data. Kwa hiyo uchanganuzi huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya maelezo. Data zilizokusanywa kutoka riwaya ziliteuliwa na kupangwa ili zichambuliwe kwa urahisi. Uchunguzi huu wa kina uliwezesha mtafiti kuhakiki kwa makini vipengele vya ukahaba vinavyojitokeza katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* na jinsi vinavyosaidia kuwasawiri wahusika kama makahaba.

### Vifaa vya Ukusanyaji wa Data

TUKI (2004) wanafasili data kuwa ni taarifa au takwimu ambayo hutumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja fulani. Vifaa vya kukusanyia data ni vifaa mbalimbali ambavyo hutumika katika kukusanya na kuhifadhi data za utafiti. Katika harakati za kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alitumia vifaa mbalimbali kama; shajara na kumpyuta mpakato.

### Kompyuta Mpakato

Kompyuta ni mashine ya kielektroniki ya kuhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa, kukokotolea na kuongoza mitambo. Pia, kwa upande wa kompyuta pakatwa, hii ni aina ya kompyuta inayoweza kubebeka kwa urahisi kutoka sehemu moja hadi nyingine ambayo huweza kupakatwa. Katika utafiti huu, kompyuta pakatwa ilimsaidia mtafiti wakati wa kuandaa pendekezo la utafiti, kuhifadhi data zilizokusanywa, kuhifadhi data na kuandika ripoti ya utafiti. Aidha, Kalamu na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

karatasi ni vifaa vya asili katika ukusanyaji wa data ya utafiti. Bila shaka vifaa hivi vitaendelea kutumika kwa miaka mingi ijayo. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia daftari na kalamu ambavyo vili msaidia katika kuhifadhi kumbukumbu za uchanganuzi wa ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*.

**Mbinu za Uchanganuzi wa Data**

Kwa mujibu wa Omari (2009) uchambuzi wa data ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma kazi ya fasihi kwa lengo la kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo na kadhalika. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo ilisaidia kujibu maswali ya utafiti unaohusika. Katika utafiti huu, Mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo katika kuchanganua data za utafiti kwa kuwa data za utafiti huu zilikusanywa kwa mkabala usio wa kiidadi, pia uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kiuthamano. Kutokana na hali hiyo data zilizokusanywa kutoka riywaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* ziliwekwa katika makundi na kisha kuwasilishwa ili kuweza kufikia malengo mahsusi ya utafiti huu.

## UFAFANUZI WA RIWAYA ZILIZOTEULIWA

**Riwaya ya *Nyota ya Rehema***

Riwaya ya *Nyota ya Rehema* iliandikwa na Mohamed S. Mohamed mwaka 1976. Mohamed Sulaiman Mohamed alizaliwa tarehe 5 Octoba 1943 kijijini Koani katika sehemu ya kati ya kisiwa cha Unguja. Riwaya hii imejikita katika mapenzi na ukahaba. Imeakisi mandhari ya kisiwa cha Unguja huko Zanzibar. Ina sura kumi na moja kwa utaratibu vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kutakasa na kukosoa jamii iliyokwamia katika shughuli za ukahaba, kukata tamaa na kuoza kimaadili ili iweze kupambazuka na kuchomoza kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, kuepukana hali ya unyonge. Mohamed Sulaiman Mohamed anasawiri wahusika wake kama makahaba wanaoshiriki ukahaba kwa ajili ya kupata pesa, Mohamed anazingatia sana kipengere cha ukahaba wa kupata fedha bora kuliko ule wa kuridhisha nafsi kwa hiyo nadharia ya umaksiimeyotumiwa na mtafiti inaifa kazi hii kiuhakiki.

**Riwaya ya *Ndoto ya Almasi***

Riwaya ya *Ndoto ya Almasi* iliandikwa na KenWalibora, mwaka 2006 na imejikita katika kuonyesha hali ya misukosuko ya maisha yanayomkabili mhusika mkuu wa riwaya hii aitwaye Almasi. Riwaya hii imeakisi mandhari ya usasa ambapo ina sura kumi na tatu zilizopangiliwa vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kudhihirisha vikwamizi vya maisha vinavyomkumba mwanadamu na kumkataza kutimiza ndoto yake katika maisha na vikwamizi hivi vinajikita katika kipengere cha mtindo wa kisasa, utamaduni, na masuala ya kijamii kama vile ndoa, mapenzi na kazi. KenWalibora amewasawiri wahusika wake kama makahaba kwa kuzingatia kipengere cha kukidhi nafsi badala ya kupata fedha kwa hiyo, nadharia ya utekelezi imeifaa kazi hii kiuhakiki.

**Usawiri wa Ukahaba katika Riwaya Teule**

Sehemu hii inajadili lengo mahsusi la kwanza ambalo ni kubainisha usawiri wa ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya za *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi ambazo* ni riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu. Uchambuzi wa maudhui wa riwaya hizi umezingatia dhamira mahususi inayohusiana na utafiti huu ambayo ni “Ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi”*. Uchanganuzi wa dhamira hizi umefanywa kwa kutumia nadharia ya utekelezi na umaksi ambazo zimemwongoza mtafiti kujua ukweli kuhusu ukahaba na athari zake kwa wahusika wenyewe. Data za sehemu hii zimekusanywa wakati mtafiti alipochambua na kusoma kwa makini riwaya ya *Nyota ya Rehema na* riwaya ya*Ndoto ya Almasi* ambapo katika uchanganuzi huo mtafiti analenga kubainisha usawiri wa ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya zilizoteuliwa.

***Uchambuzi wa Riwaya ya Nyota ya Rehema***

*Nyota ya Rehema* ni riwaya iliyoandikwa na Mohamed S Mohamed, ambayo ilichapishwa mnamo mwaka 1976. Kwa ujumla riwaya hii imebainisha masuala ya mapenzi na ukahaba yaani mapenzi ya dhati na yale ya bandia. Hali

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

inayooneshwa katika riwaya hii inaakisi mandhari ya kisiwani Unguja ambayo pia yanaweza kuhusianishwa na jamii mbalimbali za kiafrika. Riwaya hii ina jumla ya sura kumi na moja zilizopangiliwa vyema katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa wasomaji wake. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kubainisha ukahaba kama unavyojitokeza katika nyanja mbalimbali za kijamii kama vile ndoa, familia, kazi, kiuchumi na kiutamaduni pamoja na athari za ukahaba. Riwaya hii inawasilisha mivutano ya maisha yanayomkabili mhusika mkuu wa riwaya hii Rehema. Rehema ni binti kifungua mimba wa Fuad na Bi Aziza ambaye alizaliwa chini ya familia yenye Utajiiri wa hali ya juu maana yake alikuwa na nafasi kamili ya kutunzwa vizuri na bila mashaka yoyote yanayohusiana na uchumi kama vile ukosefu wa malazi, chakula, ada za shule na na haki yoyote inayompasa mtoto. Lakini punde si punde, maisha yakamgeukia kinyume Rehema; akakabiliwa na msururu wa changamoto na pengine ungemwona ukafikiri kuwa yeye ni yatima. Fuad babake Rehema kitendo cha kumuoa mke wa pili Bi Adila ndicho kilichokuwa chanzo cha mashaka haya yote yaliyomkabili Rehema katika pilikapilika za maisha.

Fuad amamwagia mapenzi yake yote Bi Adila na kumsahau yule mkewe wa kwanza Bi Aziza mamaye Rehema si hivyo tu, bali anamlazimisha kuhamia kijijini Ramwe na huko ndiko Bi Aziza alikofalikia juu ya kihoro cha mapenzi yaani ukosefu wa mapenzi ya mumewe pamoja na kuangukia bafu la fikra za kiisaikolojia kila mala kwa kumwona Bi Adila akifurahia katika mali ambayo msingi wake aliutolea jasho kubwa. Hapo basi baada ya Bi Aziza akafa, Rehema akaanza kuishi na Bi Adila mamayake wa kambo aliyemtesa hadi akakimbia nyumbani na kutoroka usiku wa manane na kuelekea nyikani pahali alipokuwa hajui. Hapo katika hali ya mbalamwezi, akapokewa na bwana mmoja aliyemkaribisha na kumpa malazi. Punde si punde, alipotoka huko akaelekea mjini ambapo aliwakuta marafiki zake Ruzuna, Chiku na Kidawa wakifanya ukahaba kama biashara yao ya kila siku katika mitaa na vishororo vya mji wa Topea, akaishi nao kwa siku kadhaa na baadaye akapata bahati ya kufanya kama Yaya Kwa Bwana Mansuri na mkewe Bi-Rose. Rehema alitimiza kazi yake ya uyaya pamoja na kujiingiza katika dimbwi la ukahaba na bwana Mansuri baada ya Mansuri kumpa zawadi kadhaa wa kadhaa kama vile kumnunulia nguo zilizojaa mvunguni mwa kitanda. Hii ndiyo sababu imeyomhimiza mtafiti afanye uchunguzi juu ya sababu zinazomfanya mwanadamu afanye ukahaba.

### *Usawiri wa Ukahaba katika Nyota ya Rehema*

Ukahaba katika riwaya hii halikusawiriwa kwa kina kama ilivyo katika kazi za kifasihi. Usawiri wa ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*unajitokeza pale ambapo mwandishi anawaonesha wahusika wake; Ruzuna Chiku na Kidawa wakifanya mapenzi yasio ya dhati yaani yale ya bandia mitaani huku wakiiuza miili yao ili wapate fedha (uk 41). Pia, Rehema mwenyewe anafanya ukahaba na bwana Mansuri ambaye ni mwajili wake baada ya Bi-Rose mke’we kuondoka na kwenda kazini, Bwana Mansuri anajifanya kama vile ana homa ya malaria na Rehema anarudi kuomba msamaha kwa makosa aliyokuwa amefanya siku zilizotangulia hapo ndipo anaposhikiwa mkono hoberahobera na akanyanyuka hadi kitandani na hapo pilika pilika za ngono zikaanza (uk. 74). Kama nadharia ya matafiti ya utekelezi, ni kawaida kwa wapenzi wa nje ya ndoa na ni jambo rahisi kwa mtu kumwambia mpenzi wake kuwa anampenda sana hata anampa zawadi za kuipambazusha hamu, motisha na hamsa ya mapenzi na jambo hili hasa hujitokeza katika jamii nyingi za kiafrika maana lina uhalisia fulani.

Maisha ya kawaida ya jamii zetu, kuna jinsi wanawake wasivyowaamini wanaume wakati wasipokuwa nao kama vile wakienda kwa safari kwa hufikiri sasa wameelekea kwenye ukahaba na tatizo hili limewafanya wanandoa kutamauka na kuhisi uchovu mkubwa na kuangalia ndoa kama mzigo usiobebeka. Kwani mara nyingi wanaume matajili au mashugadadi huwashawishi wasichana wadogo kwa kuwapa kazi au zawadi ili wafanye ngono nao na ajili kubwa hapa huwa ni kuridhisha miili yao. Kwa mfano, tunamuona bwana Mansurianavyouona rahisi kumnunulia Rehema zawadi za makanzu ghali sana ilhali kwa yule mkewe Rasmi Bi Rose zawadi huwa haba na pengine hazipo suala hili pia hujitokeza katika jamii zetu maana nadharia ya utekelezi ya kisiosholojia inaifaa kazi hii kwa sababu kazi za fasihi hueleza picha halisi yote iliyo katika jamii bila kuficha. Tumeona jinsi wanaume wanavyokwepa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

kuwasaidia wanawake wanaofanya nao ukahaba hata pale wanapokabiliwa na shida za aina yeyote. Kwa mfano, Wakati Rehema anapofika kwa marafiki wake Chiku, Ruzuna na Kidawa pale mjini, wanamsaidia kwa kumpa malazi kwani wana vyumba viwili wanamkaribisha na bila kumtoza malipo yoyote ya malazi ingawa maisha ni ya mjini ambapo kupata kila kitu ni malipo kwanza.

> *Chiku kwa mara ya kwanza kumchunuka Rehema. Alivuta bweta lake lililokuwa chini ya mvungu,na kumpa Rehema mavulia ili ajishikize.Rehema alimshukuru ingawa kanzu zilikuwa fupi na pana kuliko mwili wake, Zilikuwa afadhali kuliko serunialiyoichukuwa kwa…..kwa……jina lake lilimtoka. Usiku alikalibishwa juu ya kitanda cha mmoja wapo kati ya wawili waliolala chumba chenye vitanda viwili halikadhalika hakudaiwa mchango wa chungu cha ujima wala wa kodi ya nyumba* (Uk 46).

Zaidi ya hayo, rafiki zake Rehema wanamsaidia kupata kazi kwa bwana Mansuri, kazi ambayo wote wanakubariana na kuamua wampe nafasi hii ashughulike nayo afadhali wao waendelee na kazi zao za kuuza miili yao ili wapate riziki. Kwa mfano:

> *……haukupita muda mrefu isipokuswa Ruzuna, mtu wa nyendo nyigi, alimretea habari kuwa bwana mmoja wa majumba yam awe alitaka mtu wa kazi.Ingawa kulikuwa na mjadala kati ya wenyeji watatu: Ruzuna alitaka achukue nafasi ya kazi ili aweze kutoa mchango kama wenzake; Kidawa alipenda hiari iwe ya mwenyewe. Chiku hakuona kwa nini Rehema afanye kazi ya nje ilhali aliweza kulichukuwa jiko na wao wakamchukuwa yeye; hatimaaye iliamriwa, juu ya Chiku kusema'posimo',kuwa Rehema akasikilize masilahi ya kazi hii akiona ina mafao, vyema; akiona haina , dunia wasaa! alisema kidawa. Kweli alithibitisha Ruzuna, riziki mafungu saba.*
>
> *Kiguu na njia hadi majumba ya mawe……kwa bwana Mansuri na Bi-Rose……………*

Dondoo hilo linatubainishia kuwa wahusika hawa makahaba wanamsaidia Rehema katika kwa sababu ana tabia zinazofanana na zao wenyewe maana kazi yao inayowafanikisha kwa kuwapa riziki ni kuuza miili yao. Hali hiyo pia imo ndani ya jamii zetu makahaba husaidiana katika masuala mbali mbali ya dunia pengine huunda vikundi vya kutoleana michango ya pesa na maendeleo ya kila aina. Hata kuna makundi mengine katika jamii zetu wenye tabia zinazofanana na hawa daima husaidiana na kuwashabiki wakati wa ama changamoto au sherehe fulani. Makundi haya ni kama vile; walevi, vijana, wakulima, wezi, wacha mungu na makahaba kama tumevyoona.Kulingana na hadithi hii tunaweza kuona kuwa mara nyingi wanaume wanaotembea na wanawake kwa njia ya ukahaba, wanafanya hivyo kujiridhisha hisia za miili yao kwani hawako tayari kufunga ndoa na wanawake hao. Kishtainy anaeleza kwamba wanawake au wanaume wengi wanaojishirikisha katika ukahaba ni wale ambao wanaishi maisha ya umaskini katika jamii na wale wakwasi wanaolenga kuridhisha nafsi zao kupitia ukahaba.

Hata hivyo, kuna wanaume wengine wanaokosa kutimiza walivyowahidi wasichana kabla ya kufanya ngono nao lakini wakilala nao na kufanya ngono, huwapendi tena kwa sababu kabla ya hayo, walikuwa wakisindikizwa na uchu sio mapenzi ya dhati (Muga, 1980). Kutokana na hali hiyo, uchanganuzi wa mtafiti unaonesha kwamba wanaume wengi hawako tayari kufunga ndoa na wanawake waliofanya nao ukahaba kwa sababu kuu mbili. *Kwanza*, wanaume wengi wanaotembea nje ya ndoa hufanya hivyo ili kutekeleza matakwa ya hisia za miili yao tu mfano mzuri hapa ni ule wa Bwana Mansuri na Rehema, Baada ya kufukuzwa kazini, Mansuri hakumjali tena. Hivyo wanaume kama hao kwao kuoa si jambo muhimu bali ni mzigo wa kuhudumia familia. Pili, baadhi ya wanaume hukataa kufunga ndoa na kahaba mwenzake kwa sababu kuoa kahaba anayejulikana ni kitendo cha aibu au fedheha katika jamii. Kwa hiyo wanakataa kufunga ndoa ili kukimbia aibu kwa kuonekana wameoa wanawake wasio waaminifu.

### *Wahusika Wanaojihusisha na Ukahaba*

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*mwandishi amewachora baadhi ya wahusika wake wakijihusisha katika taasisi ya kahaba kama vile; Rehema, Chiku, Ruzuna, Kidawa na Mansuri. Tuangalie wasifu wa wahusika hao katika sehemu zitakazofuata.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

**Rehema**

Rehema ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*. Rehema ni msichana anayekulia katika maisha ya magumu ingawa kuna na nyota za maisha zinazomkabili tangu utotoni. Kiwango cha nyota zinazomkabili Rehema ni sawa na changamoto zinazomkabili maishani. Ni Bintiye bwana Fuad na Bi Adila. Alizaliwa wakati wa hali ya maisha ya utajili ilipokuwa imepanda kilele lakini punde si punde mama yake wa kambo Bi Adila akafanya juu chini ili Nyota zake Rehema zibadilike na kuwa laana. Asingalikuweko mama yake wa kambo huyu, asingaliteseka na kuangukiwa msururu wa misiba mmoja baada ya mwingine, kwa hiyo, Bi-Adila ndiye chimbuko la mchafuko wa maisha ya Rehema na yote yaliyomkabili mwaishani mwake. Kwa mfano, hapo, mwanzoni Bi Adila anampendekezea mumewe Fuad awafukuze Rehema na Mamaye Bi Aziza watoke nyumbani kwao asiwaone tena kwani amejaa debe la chuki dhidi ya hao wawili huu ni wakati Rehema angalipo mchanga. Kwa mfano:

> *….Sina tena cha kusubiri; Bi-Adila aliweka wazi;tumbolinanikeketanikiliona lile toto lake la haramu likicheza na mwanangu Salma na wewe mja wa huruma huna ufanyalo……Fuad alichukuliwa na fadhaa, ilimwia vigumu kumrithi Adila, lakini vigumu zaidi kumvunja. Ingawaje,fikra mwafaka ilikuja kumtaznua*
>
> *"Sikia mpenzi Adila; alinena, tutamwondoa huyu Aziza pamoja na huyu mwanawe tumpeleke huko katika shamba langu la Ramwe na wewe hutawaona tena. Ngonjea…….Hamisi! Hamisi! kijana aliyekuwa akipangusa Land Lover alikuja mbio. Hamisi, nenda moja kwa moja mpaka Ramwemwambienakoa,Mzeepongwa, asafishe nyumba nje na ndani, fanicha zote azianike, nayeyeasiondoke wiki hii, aliamuru Fuad huku akimtupia jicho mkawe lenye kupima athari za maneno yake….(Uk 2)*

Kulingana na dondoo hili, twaona chanzo cha Rehema angalipo mchanga ambapo anafukuzwa nyumbani kwao juu ya mchango wa ckuki ya mama yake wa kambo Bi Adila ambaye anawachukia sana ingawa alikuwa mke wa pili. Hapo ndipo Nyota yake Rehema inapoanzia kubadilika kinyume. Punde si punde baada ya kufika huko Ramwe, mamake akaaga dunia juu ya kihoro cha mapenzi ya mumewe wakati Rehema angalipo mchanga wa kama miaka sita. Aliporudishwa kuishi na BiAdila papo hapo mchafuko wa maisha ya Rehema ulipanda kilele na hatimaye akaamua kutoroka nyumbani. Kitabia; kwanza, Rehema amechorwa kama mfanyi kazi kwa sababu twamwona pale kwa bwana Mansuri na mkewe Bi-Rose, akifanya kazi ya yaya kwa kumlea mtoto wao pamoja na kufanya kazi zote za Nyumbani kama vile kusafisha vyombo vya kulia, na kazi zote za nyumbani. Ni uwajibu wake kumlea mtoto na Bi-Rose asipokuwepo nyumbani, Rehema anatakiwa kumtayarishia kila kitu bwana Mansuri ili shughuli zote za nyumbani zitimizwe taratibu. Pili Rehema amesawiriwa kama Kahaba. Wakati anapokutana na rafiki zake Ruzuna, Chiku na Kidawa ambao ni mafundi katika shughuli za kuuza miili yao kwa ajili ya pesa, naye Rehema anafunzwa tabia hizi za kufanya ngono ili apate riziki. Kwa mfano, tunamwona akifanya ngono na Bwana Mansuri ili apate kusamehewa na aendelee na kazi zake bila tatizo. (Uk 74):

> *…Ah,hiyo ndiyo iliyokuchukua kuliko zote. Mansuri huku akinyanyuka na kumsongelea Rehema. Alishika mikono yote miwili kwa ghafula ba bila Rehema kutaraji, Mansuri aligusisha midomo yake kwa shavu la Rehema, na kuiondoa ….(Uk 63)*

Katika dondoo hili Rehema anakubali zawadi zake bwana Mansuri, na suala hili ndilo lililofanya kama jarada Kufanya ukahaba kati ya hawa wawili. Lengo la mwajili huyu kumnunulia zawadi zilizojaa mvunguni mwa kitanda cha Rehema lilikuwa la kufanya mapenzi naye na hapo tunaona mwishoni lengo Lake lilitimizwa. Ingawa Rehema anafanya ukahaba na Mansuri, haikuwa hiari yake ya mapenzi ya dhati bali ni uchochezi wa shida za kiuchumi kwa sababu Rehema hakuwa na uwezo wa kujinunulia mahitaji hayo yeye mwenyewe maana alikuwa katika hali ya unyonge. Hapo basi Mansuri ambaye ni bepari anapandia kwenye nguzo ya uwezo wake wa kiuchumi kuridhisha mwili wake na yule Rehema mnyonge mwenye debe la mahitaji.

**Bwana Mansuri**

Mansuri ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, mwenye nywele za singa zilizoliwa na upara katikati, pua yenye mgongo, na macho

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

manene, mekundu yenye wasiwasi. Pia ni mfanyibiashara za namna kwa namna. Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, bwana Mansuri amesawiriwa kama mtu mwenye huruma kwa sababu tumamwona Rehema alipofika kwake nyumbani tayari kufanya kazi, anamwonea huruma kwa kumpa fedha za kununua viatu ili apate hamu ya kufanya kazi zake bila kukubali shingo upande. Papo hapo, Rehema anaondoka kwa mbio na kuelekea dukani kununua viatu. Mansuri anasawiriwa kama mhusika kahaba katika riwaya hii; kwa mfano, sili binafsi inayomsihi kumnunulia zawadi za nguo Rehema mwajiliwa wake ili kujenga daraja la kumuingilia kimapenzi. Baada ya kuzileta nyumbani, anamwagiza azivalie papo hapo huku Mansuri akiangalia na jicho pekuzi:

> *".. …Ah,hiyo ndiyo iliyokuchukua kuliko zote. Mansuri huku akinyanyuka na kumsongelea Rehema. Alishika mikono yote miwili kwa ghafula ba bila Rehema kutaraji, Mansuri aligusisha midomo yake kwa shavu  la Rehema, na kuiondoa ….''(Uk 63)*

Kwa mara nyinine, Mansuri anadhihirishwa kama Kahaba mtendaji pale anapojifanya kuwa yeye ana homa kali. Alibaki kitandani na punde si punde, Rehema akiingia katika hali ya kumwomba msamaha kwa makosa aliyokuwa amemfanyia hapo awali kwa kumwuma bega katika mchakato wa kumlazimisha waingie kitendo cha mapenzi lakini hatua hiyo ikamwangusha katika mdomo wa chui;

> *Manasuri aligeuka kumtazama Rehema pasi na kumsemesha lolote, macho yake yakionyesha mtisiko wa homa. Rehema katika hali ya woga na kubwana na hisia ngeni asiozozijua, alisimama mbele yake kama mpumbavu, mikono yake kaishika pamoja chini ya kitovu tone za machozi zikichungulia katika pembe za macho yake. Mansuri alitoa miguu yake chini ya blanketi alilojifunika, akanyanyuka na kumshika mkono Rehema,kimya, kimya, pole pole, na kumpandisha kitandani kwani alijua Rehema akitaka nini……* (Uk 74).

Kulingana na dondoo hii, Bwana Mansuri anatambulika kama mhusika kahaba anayependa sana kujishughulisha katika matendo ya ukahaba, kwa sababu hapo mwanzoni anaanza kutega mitego yake ya kumzawadi Rehema kwa ajili ya kumsawishi kimawazo. Kitendo hiki kina uhalisia na jamii kwa sababu wanaume na wanawake pengine matajili huwanunulia zawadi ghali sana ili wanawake wasawishike kimawazo na kufikiri ya kwamba hayo ni mapenzi ya dhati kumbe ni ya bandia, baada ya kutimiza lengo kuu lile lile la kuridhisha miili yao,na baadaye huwatupa kama maganda ya njungu. Mara nyingi watu wa aina hii huitwa "mashugadadi" na "mashugamumy". Riwaya hii inamchora bwana Mansuri kama kiwakilisho cha wanaume kama wao ambao wapo katika jamii yangu (Masebo na Nyangwine, 2003). Wanaume hao huwapenda wanawake kwa ajili ya kuwatekelezea matamanio yao ya kimwili tu, lakini hawako tayari kuwasaidia wapenzi wao wanapopatwa na matatizo. Kwa mfano Baada ya Bi Rose mkewe Mansuri kutambua sili hii akamfukuza Rehema na hapo hatumuoni tena Mansuri akifuatilia Rehema kumsaidia Chiku

Chiku ni mmoja wapo wa wahusika waliomo katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, ni mwanamke mzima lakini anamwacha mumewe na kaamua kuenda mjini Topea ili afanye ukahaba na wanaume wengine kwa lengo la kupata fedha. Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, Chiku anasawiriwa kama mhusika kahaba ambaye anakitegemea kitendo hiki cha kufanya ngono na wanaume wengine ili apate pesa. Kwa mfano tunamwangalia Rehema akiwakuta ana kwa ana bila aibu katika chumba walichokuwawametengenezea wageni (wateja) wanaume kwa ajili ya kufanya ukahaba:

> *……….Bila kujitambua,Rehemaalisongelea karibu na mlango wa chumba na kurekebisha jicho lake katika ufa wa mlano na kumwona chiku paaoja na shujaa wake aliyeshinda mapigano ya hivi karibuni wameumana.Nguvuasizozimudu zilimtwaa Rehema*
>
> *alitetemeka……….alihaha…..alitapatapa….na hata alipoweza kuligundua jicho mlangoni moyo wake ulikuwa ukishindika kwa kasi. Upesi upesiuliposukia chumbani na kujitupa nyuma ya kidawa aliyekuwa akikoroma……. (Uk 72)*

Kulingana na dondoo hii, twahakikisha kuwa Chiku ni kahaba hodari yeye ndiye anayebadilisha wanaume kama sharti, yaani kila siku kuna ratiba ya ngono. Hopo tunatambua kwamba nadharia imeyotumiwa kuhakiki kazi hii inaifaa, wanaume (wateja) ambao ni mabepari hutumia mali yao

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

kuridhisha utashi wa miili yao kwa kununua hawa wanyonge. Changamoto hapa kwa wanawake ni ukosefu wa kujiweza kiuchumi au kuwa na haja ya kuwa na mapato zaidi ya mishahara yao, hutoa miili yao kwa wale walionacho au matajili. Mwaandishi wa riwaya hii amemchora Chiku kama mlipiza kisasi kwa sababu hapo awali, mumewe alifanya ukahaba na wanawake wengine na kwa hiyo naye akaamua kumlipiza kisasi mumewe ili naye ayahisimauminvu ya usaliti wa ndoa ili naye apate hasira kama vile alipomfanyia. Mwandishi hapa hutoa wazi wazi kuwa wanawake wengine hujiingiza katika taasisi ya ukahaba baada ya ndoa zao kuvunjika, hapo basi kwa utamaushi mwingi hushiriki ukahaba kama mkabala wa kujiliwaza.

**Kidawa**

Kidawa naye ni mmoja wapo wa wahusika wanaojitokeza katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*. Kwa upande wa wasifu, mwandishi anamsawiri kama Kahaba mpenda maisha ya mjini kama kazi zao makahaba, Chiku naye ana imani kwamba kupata riziki ni kuanza kujiuza kimwili halafu hapo basi maisha yaanze kuendelea kiutambalale.Kwa hiyo naye anajiingiza katika shughuli za ngono kama kazi yake ya kawaida, kwa mfano:

> *….. mara tu walipong'oka mle chumbani Kidawa alimshika mkoono mgeni wake wakaingia katika chumba lilichoachwa kwa wapiganaji,kiti cha marimba kikawekwa kuchukua mali pa peteiliyovunjwa na wawili wakashughulikia na yao"*(Uk 46).

Dondoo hili lahidhirisha kwamba Mohamed Sulaiman Mohamed amemsawiri mhusika huyu kama mwenye uimala katika ukahaba pia, ambaye ametua ukahaba kama biashara yake. Kulingana na smart (1976), baadhi ya wanawake hushiriki ukahaba sio kwa sababu ya kutojiweza kiuchumi bali kwao, ukahaba ni biashara ya mazoea ya kila siku.

**Mtazamo wa Mwandishi kuhusu Ukahaba**

Katika kuhakiki Riwaya ya *Nyota ya Rehema* tumeona kuwa mwandishi Mohamed Sulaiman Mohamed amemchora mhusika Mansuri kama mhusika kahaba baada ya kufanya mapenzi na Rehema. Sababu ya kufanya ukahaba naye si kwa ajili ya kumwonea mapenzi ya ukweli au hakutaka chochote kutoka kwa Rehema, bali ana lengo la kuridhisha mwili wake na kuustarehesha (uk.75). Kwa upande wake Rehema naye pia hakusindikizwa mapenzi ya dhati ili apate kufanya ukahaba na Mansuri bali alisindikizwa zile zawadi alizopewa hapo mwanzoni na mwajili wake Bwana Mansuri. Pili, Rehema alitimiza ombi la Bwana Mansuri alilokuwa anamdai kila siku kwa ajili ya kuhifadhi kazi yake. Hapo mwanzoni, Mansuri alijaribu kumshika kwa nguvu na kumlazimisha katika mapenzi lakini Rehema aliposhindwa nguvu na hili jiumelembamba akaona heri kumuuma na hapo akamponyoka. Rehema alipokumbuka kisa hiki akadhani endapo atapoteza kazi yake basi akaamua kukubali kufanya mapenzi na Mansuri. Mohamed S. Mohamed katika Riwaya hii anasawiri ukahaba kitendo kinachosababishwa na ukosefu wa uwezo wa kiuchumi haswa kwa upande wa wanawake.

Kulingana na nadharia ya utekelezi na Lowry (1974:198), huelezea kwamba ukahaba husababishwa na hali ya kiuchumi. Kwa hiyo, mhusika kama Rehema anasindikizwa na hali hiyo katika vitendo vya ukahaba hata hapo mwishowe anatamauka na kukosa msada wa kujichunga kingono maana anaanza bishara ya ukahaba wazi wazi na wanaume wengi hapo mjini Topea baada ya kufukuzwa kazini kwa kitendo hicho. Kitendo hiki kinatokea baada ya Bi Rose mkewe Bwana Mansuri kuwakuta ana kwa ana kaikukurukalia katika dimbwi la mapenzi na akamfukuza kazini Rehema (Uk 77). Hali hivyo,mwandishi hakutoa suluhisho bayana kuhusu ukahaba katika riwaya hii. Wasomaji hawapati mafunzo mwafaka kuhusu suala hili kwani mwandishi halichambui kwa undani na kuonesha kwa kina athari za ukahaba zilizowapata wahusika kama Ruzuna, Chiku na Kidawa bali anaendeleza mhusika mkuu Rehema katika majadiliano yake. (Uk 80).

Mwandishi, anadhamira ya kudhihirisha kwamba familia zisizo imala huwapa malezi mabaya watoto, wanakua na mtazamo hasi kuhusu maisha halafu huimalizia katika taasisi za ukahaba kama njia moja ya kulipiza kisasi cha mapenzi waliyokosa kupewa na wazazi wake utotoni. Kwa kuuchukulia kabisa mfano wa mhusika Chiku, mwandishi anaonesha kuwa makahaba wengi katika vichochoro vya miji huwa ni wale ambao ndoa zao zilivunjika hapo basi hukata tamaa na kuanza kuuza miili yao ili wapate

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

riziki. Chiku naye mambo yakamwendea hivyo hivyo akaamua kujiunga katika taasisi ya ukahaba mjini topea. (Uk80). Kwa kiasi kidogo, mwandishi anadhihirisha mapenzi ya ukweli maana 'mtenda mema hulipwa mema'. Baada ya Rehema kuzunguka kote, alimkumbuka bwana mmoja kwa jina la Sulubu Nguvumali ambaye alimwonyesha huruma na mapenzi ya ukweli wakati alipotoroka nyumbani akaelekea nyikani sehemu alipokuwa hajui usiku wa mabaramwezi. Kwa ujumla, mwandishi amejibidisha kuzingatia nadharia ya umaksi katika kazi yake kwani ameweza kuisawiri jamii kifasihi na kuelezea changamoto za maisha ya kikahaba katika jamii ingawa hakuweka bayana madhara ya ukahaba huo.

## Uchambuzi wa Riwaya ya *Ndoto ya Almasi*

Mhusika mkuu Almasi katika riwaya hii ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule ya upili St. Joseph's. Ni mtoto wa pekee wa kiume wa mzee masasi na Paulina. Almasi ana ndoto yake anayotaka kutimiza katika maisha yake yaani ndoto ya kuwa mtangazaji mazingira redioni lakini anakumbwa na msururu wa vipingamizi vya maisha vinavyomzuia na kumbwamisha ili ndoto yake isitike. Katika harakati zake za kutimiza ndoto yake, anfanya matendo ambayo yalikuwa athari kubwa dhidi ya nafanikio yake tokea siku sikuu alipojiunga na shule ya upili, miongoni mwa makosa aliyofanya Almasi ni kama vile, kufanya mgomo shuleni, kuamua kuacha shule, ukahaba, na maamuzi mabaya yasioendana na ndoto yake. Kando ya makosa anayojifanyia yeye mwenyewe, hadhi yake ya kuwa na familia isiyo imala ilimtatiza sana kwa sababu tunamwona babake Masasi anatengana na Mkewe Paulina na kumwoa mama Chebosio mkewe marehemu Chifu Cheboi. Aliporudi nyumbani kutoka gerezani, hata anapata matata na babake Mzee Masasi na anatoroka nyumbani kwa msada wa pesa za nauli mamake Paulina alizokopa kwa Mangdelina Makabila, anaelekea mjini na kumfikia dadake Naliaka lakinni baada ya muda mfupi wanatengana kwa ajili ya Almasi kutotaka kumbebesha mzigo mkwewe. Anaingia mjini na kuanza kufanya kazi ya ubawabu ili kupata riziki. (Uk 104).

## *Usawiri wa Ukahaba katika Ndoto ya Almasi*

Mwandishi KenWalibora katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* ameusawiri ukahaba kwa namna moja. Mwandishi huyu amewachora wahusika wakijihusisha na ukahaba kutokana na sababu moja tu ambayo ni ya kuridhisha miili yake sio kwa matarajio ya kitu chochote zawadi au fadhatofouti na Mohamed S. Mohamed ambaye aliwasawiri wahusika wake kwa kuzingatia kipengere cha Pesa na zawadi kama sababu ya kuwashiriki kitendo cha ukahaba wahusika wake katika riwaya ya Nyota ra Rehema. Anawaonyesha jinsi wanafunzi wa elimu ya juu wanavyojishirikisha na ukahaba kutokana na tamaa ya kuilidhisha miili yao. Kwa mfano, katika dondoo alifualilo (uk. 33), mwandishi anaonyesha kiasi cha ukahaba wa wanafunzi shuleni St. Joseph's:

> *………wasichana wa kidato cha kwanza waliokuwa wamejaa haya na kutojiamini walikuwa shabaha ya wavulana wakubwa wenye ukware wa Mbwa koko. Na walikuwa mawindo rahisi. Nyakati za kudurusu madarasani usiku zilikuwa na viroja na vioja. Wavulana hao wakiwatoa wasichana mmoja mmoja na kuwaburura nje kama kondoo wanaopelekwa machinjioni.Wafanyaje wasichana wa watu dhalili pale walipo?Almasi alishangaa usiku mmoja alipofumania mvulana mmoja akihema na msichana akilia karibu na safu ya vyoo. Siku nyingi baadaye Almasi alizoea kushuhudia visa kama hivyo".*

Katika dondoo hilo mwandishi anawaonyesha kiasi ambacho wanafunzi wa shule ya upili St. Joseph's wakishughulikia ukahaba hali kama hii ni hatari sana katika utendaji wa wanafunzi. Mwandishi adhihirisha mandhari yaliyokuwa maana kwamba uozo wa maadili ulikuwa umepanda kilele kwa sababu hali kama hii huonyesha kweli hapakuwa na walezi wanaoajibika kukamilisha malezi bora ya wanafunzi. Maandishi haya huakisi kuwa ukahaba katika taasisi za elimu kama shule za sekondari, vyuo na hata katika baadhi ya familia endapo huendelezwa na ukosefu wa wazazi kutimiza uwajibu wake hapo mwanzoni wa kuwatunza watoto hasa vibarubaru jinsi wanavyostahili kujichunga kihisia na ili kukua na maadili yanayofaa katika jamii. Wanafunzi walio na tabia mzuri huathiriwa na tabia mbaya kwa kuishi na wale walio na tabia mbaya, tumamwona naye Almasi anaathirika kwa kuzoea vitendo vya ukahaba. Kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

hiyo inawafaa walezi watekelezeuwajibu wake ingalipo mapema ili kuepukana uharibifu wa watoto na jamii nzima. Kwa mfano, walipoendelea na tabia hizo walimalizia wakiichoma nyumba yake mwalimu mkuu Kipsung Patrick na kumuua kwa sababu alichelewa kuanza harakati za kurekebisha tabia za wanafunnzi, na sasa kwao wanafunzi imegeuka na kuwa utamaduni maana hawaioni kuwa tabia mbaya.

Mwandishi KenWaliboraanonyesha kuwa unachukuliwa kama kuridhisha miili sio matarajio ya kifedha, kwa mfano katika Dondoo lifuatalo, tumamwona Mzee Masai akitekwa na bakunja na mama Chebosio mkewe marehemu Chifu Cheboi. (Uk 19):

> *"Baba yuko wapi?"aliiuliza tenaMama aliinamisha uso wa kutazama sakafu ya saruji ya samadi na mchanga".*
>
> *"Ya babako ni makubwa," alisema huku anatikisha kichwa.*
>
> *"kwani kulikoni?"*
>
> *"Amehamia kwa mama Chebosio"*
>
> *"Mke chotara wa Chifu Cheboi?"*
>
> *"Marehemu Chifu Cheboi."*
>
> *"Chifu cheboi alikufa?"*
>
> *"Nyasi zimeota kaburi zima kwa sasa."*
>
> *"Chifu Cheboi!"*
>
> *"Miaka miwili mitatu imepita."*

Kulingana na dondoo hili, mwandishi anaonesha kwamba Mzee Masasi alihamia kwa mama Chebosio na kuacha familia yake kwa ajili ya kufanya ukahaba. ChambilechoLittle (1973), watu wengi huwa ma wapenzi wengi nje ya ndoa kama makahaba aua Masuria. Kutokana na hali hii, wanawake wengi wameshindwa kuvumilia tabia hiyo ya kutokuwa na uaminifu. Wengine wanadai kwamba, kuwa na mke mmoja ni kujichosha na wengine hudai kuwa ni njia moja ya kutajilika. Kulingana na desturi baadhi ya dini na jamii fulani huamini kwamba mume akiwa na uwezo wa kiuchumi, yaweza kuoa wamawakeanaowataka.

### *Wahusika Wanaojishughulisha na Ukahaba*

Riwaya ya *Nyota ya Rehema*, mwandishi amewasawiri baadhi ya wahusika wake wakijihusisha na ukahaba kwa namna ya kuridhisha miili yao. Katika riwaya hii wahusika ambao wanahusishwa na ukahaba ni kama vile Almasi, Chemtai, Chebosio Mama Chebosio, wanafunzi wa shule ya upili StJoseph's na Mzee Masasi. Katika sehemu ifuatayo, mtafiti alielezea wasifu wa wahusika waliomo katika riwaya.

### Almasi

Almasi ndiye mhusika mkuu katika riwaya hii pia ni mtoto wa pekee wa kiume wa mzee masasi na Paulina. Almasi amesawiriwa kama mhusika kahaba anayefunzia tabia hii wakati alipokuwa katika shule ya upili ya StJoseph's kidato cha kwanza.(Uk 13):

> *Wavulana hao wakiwatoa wasichana mmoja mmoja na kuwaburura nje kama kondoo wanaopelekwa machinjioni.Wafanyaje wasichana wa watu dhalili pale walipo?Almasi alishangaa usiku mmoja alipofumania mvulana mmoja akihema na msichana akilia karibu na safu ya vyoo. Siku nyingi baadaye Almasi alizoea kushuhudia visa kama hivyo.*

Dondoo hili ladhalilisha kwamba Almasi alikuwa hajui mambao kama haya lakini kwa uzoefu wa visa alivyokuwa anahusika shuleni na wanafunzi wengine wazoefu, hapo basi naye akapandwa na roho ya ukahaba iliyomrithi katika maisha yake. Katika tabia zake za ukahaba, Almasi hawapi chochote wanawake kama vile Pesa au zawadi yoyote bali, wao wanajimwagika katika dimbwi la ngono kwa ajili ya kujistarehesha na kujiridhisha kinafsi.

Mwandishi anamsawiri Almasi kama kahaba katika dondo lifuatalo *(Uk 28):*

> *Akajibwaga chali kitandani. Akatazama mtambapanya wa ensimba yake, kitanda chenyewe si kitanda kitu. Akakumbuka miaka mingi iliopita, alipotumia masalio ya kitanda cha mbao na misumari ya baba'ake akabambanya kitu mfano wa kitanda cha kamba. Akajigeuza chali kwa sauti kubwa ya malalamiko.Kilikuwa bado kipya kipya hivi- na*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

> *kipya kinyemi kingawa kidonda alipomleta msichana mmoja usiku **kula oronda.** Manzi mwenyewe wa kuliwa asibakishwe kitu ni Chebosio, binti Chotara wa Chifu Cheboi. Mkamia maji hayanywi, Amasi alishangaa, akawa natokwa tu na jasho mtawalio kama mkimbiaji wa mbio za nyika. Walikuwa katika pilika pilika za kumwamsha aliyelala katika kitanda kiliposalimu amri wakajikuta sakafuni wote waliukosa 'uronda' pamoja na kitanda,wakalala sakafuni huku wamenyamaziana kama majabali mawili yanayokingiana. Chebosio alirauka alfajilimapena na kujiendeleza zake. Kesho yake kulikuwa kazi kubwa ya kukifanyia ukarabati kitanda chenyewe.Hii ilikuwa yawezekana, kwa Almasi kukarabati kitanda ilikuwa kazi rahisi kabisa…………*

Dondoo hili, lamtambulisha Almasi kijana anayesheherekea visa vya ukahaba uliyo wa kuridhisha mwili wake sio ule wa pesa. Mwandishi ametumia mbinu ya sanaa ambayo ni kisengere nyuma cha kitendo cha ukahaba walichofanya Almasi na Chebosio hapo awali. Walipokuwa wamelala usiku wa manane baada ya kufanya ngono, kitanda kilichokuwa kimesalimu amri kikavunjika na hatimaye wakajikuta sakafuni. Nadharia ya utekelezi ambayo imetumiwa katika utafiti huu inafaa katika uelezaji wa shughuli hii yaani hawa wahusika waili wanajiingiza ukahaba kwa ajili ya kuridhisha utashi wa nafsi zao badala ya pesa au zawadi.

Aidha, katika dondoo lifuatalo, mwandishi anamsawiri Almasi kama mhusika kahaba anayesindikizwa na hisia za mwili kushiriki matendo ya ukahaba *(Uk 140-142)*;

> *Nasikia uchungu kuachana na wewe," Almasi alisema huku kijoyo kinamdunda.*
>
> *"Samahani mimi sihisi chochote kuelekea."*
>
> *"Kwa hiyo huwezi kunipa nafasi katika moyo wako?"*
>
> *"Kwa nini nikupe nafasi ?"*
>
> *"Kwa nini usinipe?"*
>
> *"Kwanza ni suala la heshima," alisema Cheboshio kwa henezi uso ameukunja kwa mazingatio. "Baba yako na mama yangu wanapendana; iwe mimi na wewe kusuhubiana?. Ni kinyume na maadili ya kijamii."*
>
> *Lakini wao wamejikosea heshima na tutawatia adabu tukipendana."………………..Chebosio akakumbuka wimbo ambao mwalimu wake wa kapsara amekuwa amemtungia-akauimba kwenye mashindano ya shule za upili kwenye makavazi ya kitaifa mjini kitale……….maneno ya wimbo huo na sauti na mahadhi ya Chebosioyakamtwa katika akili ya Almasi mchana kutwa……*

Dondoo hili laonyesha vile Almasi walipojikita katika uwanja wa mapenzi wakati wa ndoa ungalikuwa haujafika, maana mapenzi yao yalitendekea nje ya ndoa yaani. Hata katika jamii, vijna hujiingiza katika mapenzi ya aina hii na huishia wamevuka mipaka kwa sababu mapenzi yanayohusisha ngono yafaa wawe miongoni mwa wanandoa sio wale vijana baleghe ambao hawajaingia ndoa kwa hiyo Almasi na Chebosio ni makahaba.

## Chemtai

Chemtai ni mkwe wa mke wa mzee Kirwa. Mke wa pili wa mzee kirwa alikuwa tasa maana hakuwa na uwezo wa kuzaa watoto na kulingana na mila na desturi za kwao, mke akiwa tasa,anaruhusiwa kumwoa mke mwingine kwa niaba ya mumewe, hapo basi mume hutegemea mke wa mkewe ili amzalie watoto. Mwandishi amemsawiri mhusika huyu kama Kahaba kwa sababu alikuwa na watoto nane na kila mtoto alikuwa na baba'ake. Badalaya ya kumhudumu Mzee Kirwa peke yake, akaamua kuwagawia mapenzi wanaume na bila kuwabagua kisura,rangi au kabila kama inavyofafanuliwa katika riwaya. (Uk 47):

> *…..kuliwahi kuweko mzozo kuhusu majina ya watoto hao,mwanzoni waliitwa majina ya kikalenjin kama vile Kipchumba, Cheruto na Chesang hadi ikabainika kwamba madume walikuwa wa makabila mbali mbali kama yalivyo makabila mengi katika tarafa ya Cherangani. Kuna watu walioshikilia kwamba*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

*watoto wapewe majina kutoka kwa makabila ya madumemwaliomtungisha mama yao mimba.*

*kwa hiyo Chemtai akaanza kuwaita watoto hao majina kama vile Chenge, Naliaka, Auma na Nekesa, mumewe yaani mke wa pili wa mzee kirwa , akapandwa na za kwao. majina ya kigeni yalikuwa kama ndege zilizopaa katika anga za wenyewe. Majina ya wali yakarejeshwa mara moja.*

Dondoo hili linaonesha kuwa, maisha ya Chemtai yalikuwa ya ukahaba, alikuwa na uchu wa hali ya juu maana ni  Kahaba. Hapa pia, mwandishi amemsawiri mhusika huyu kwa kuzingatia kipengere cha kuridhisha nafsi, hakuhusisha kile cha ukahaba unaolenga fedha au zawadi. Mwandishi amemsawiri Chemtai kama mhusika Kahaba, kwa vile alipomwangusha Almasi katika dimbwi la mapenzi ya dharura pale mtoni alipokuwa ameenda kuchota maji akamkuta Almasi amejianika uani baada ya kuoga (Uk 68):Siyo kwamba sijawahi kumwona mwanamume katika hali hiyo," alisema kwa matani hukuumejaa bashasha.. "Elakini nimeshangaa. Hebu nisimame nikuone vizuri.

*"Huna adabu wewe!"*

*"Elakini kumbe ni kweli vile niliambiwa."*

*"Uliambiwa nini?"*

*"Kwamba wewe ni* ***weeri****vile sisi wananditunasemaga au* ***omusinde*** *kama vile nyinyiwaluyiamnasemaga.*

*"Chemtai !Ondoka hapa!"*

*"Hebu nione kidogo tu basi."*

*"Kama unataka kuona ONA basi," Almasi alisema bila kufikiria. Kisha akanyanyuka na kusimama wima.Alihisi hamaki na hawaa na wenda wazimu vimechanganyika. Chemtai alirudi kinyumenyume hatua mbili tatu kama kwamba anatoroka mnyama mwitu hatari. Ni kama hofu lakini hofu ya kisebusebu  na kijoyo kipapo. Alitua na badala ya kuendelea kwenda nyuma alianza kumkaribia tena ALmasi kwa taratibu huku uso umepigwa na pumbuazi. Almasi ayekuwa amesimama kama nguzo ya umeme, sasa alikuwa hajali wala habali Kichaa chake kimefika kileleni. Mke huyo wa mke wa Kirwa alitikisa kichwa huku kumtumbulia macho Almasi. Mke wa mke aliyerembua macho na kumnasa Almasi katika mtego wa uchu usiosikia dawa……….*

Dondoo hili ni thibitisho kuwa kweli kabisa mhusika Chemtai alikuwa Kahaba mashuhuri kwa vile anavyomtega Almasi hadi akamwangusha katika mtego wa mapenzi. Pia maapendi yale yale mtoni inadhihirisha uchu wa mapenzi wa hali ya juu na lengo kuu hapa ni kuridhisha mwili uliyo na nyota ya mapenzi sio kutarajia malipo kama vile fedha au zawadi. Kingsley ambaye ni mwanasosiolojia mwenye mtazamo wa kutekelezi amenukuliwa na Lowry (1974:220) akieleza kwamba katika jamii ya kisasa kuna sababu kadha wa kadha zinazoea kuwepo kwa Ukahaba. Kwanza, ukahaba husababishwa na ile hali ya kifedha pamoja pamoja na hali ya kuridhisha nafsi. Kulingana na mtazamo wake Mtaalamu huyu, hapa mwandishi KenWalibora amemsawiri mmhusikaChemtai kwa kuzingatia kipengere cha pili ambacho ni kuridhisha nafsi. Kama fasihi yoyote huwa ni kioo cha jamii, mwandishi ana dhamira ya dhihirisha wasomaji au jamii kuwa kuna wanawake na wanaume katika jamii zetu wanaojihusisha na Ukahaba kama burudani au kuridhisha nafsi tu.

**Mzee Masasi**

Mzee Masasi naye ni mmojawapo wa wahusika wakuu katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi*. Mwandishi pia amemsawiri mhusika huyu kama kahaba kwa visa vya ukahaba anavyoshughulika navyo kama vile  Kishtain na wenzake wanavyoeleza kuwa, kahaba ni mwanamke au mwanamume anayeshiriki mapenzi ya watu wengi, Mzee Masasi naye anashiritki mapenzi ya watu zaidi ya mmoja kwani anamwaacha mkewe Paulina na kuolewa kwa mama Chebosi mke Chotara wa marehemu Chifu Cheboi. Baada ya Almasi kurudi nyumbani, anamuuliza nyumbani mahali baba yake amekoenda lakini mamaye Paulina alikuwa ameishia maneno yaani Mzee masasi akamuacha nyumbani akahamia kwa mama Chebosio mkewe marehemu chifu Cheboi ambapo wanafanyia kahaba. Kwa mfano dondoo lifuatalo linathibitisha kuwa Mzee Masasi anashiriki ukahaba *(Uk 19)*:

*"Baba yuko wapi?"aliiuliza tena*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

*Mama aliinamisha uso wan a kutazama sakafu ya saruji ya samadi na mchanga.*

*"Ya babako ni makubwa," alisema huku anatikisha kichwa.*

*"kwani kulikoni?"*

*"Amehamia kwa mama Chebosio"*

*"Mke chotara wa Chifu Cheboi?"*

*"Marehemu Chifu Cheboi."*

*"Chifu cheboi alikufa?"*

*"Nyasi zimeota kaburi zima kwa sasa."*

*"Chifu Cheboi!" "Miaka miwili mitatu imepita."*

Dondoo hadhihirisha kwamba ukahaba ulimzidi uwezo mzee Masasi hadi akavunja kanuni ya Kiume; yaani kawaida wanaume huoa na mwanamke huolewa sio tena mwanamume kuolewa, laiki yeye akavunja kanuni ya akaolewa na kewe marehemu kwa jina la mama Chebosio. Mwandishi pia anamchora mzee Masasi kama kahaba mashuhuri anayelenga kuridhisha nafsi na kwa kuwa alikuwa ameolewa na mwanamke aliyekuwa na watoto wasio wa mzee Masasi, watoto wenyewe wanajua babake alikufa sasa je! huyu baba mpya katika nyumba ni nani sio Kahaba??. Hapo basi mzee Msasi wanamchukia kabisa kwa sababu ni kahaba (Uk 52).

*"Umekuwa kama baba lako"*

*"Ehe?"*

*" Uliambielitoke kwetu. Ndugu zangu wakitoka Mombasa wakalipata litaona cha mtema kuni"*

*"Aisee dharau kama hii haifai Chebosio."……*

Mazungumzo ya Chebosio na Almasi kama yanayodhihirishwa katika dondoo, yanaonyesha kwamba watoto wa mama Chebosio hawampendi hata kamwe yule kahaba Mzee Masasi, wanamchukia sana kwa sababu si babake bali ni kahaba, na kahaba mara nyingi hathaminiwi.

**Wanafunzi wa Shule ya St. Joseph's**

Hawa pia ni wahusika katika hadithi hii ya *Ndoto ya Almasi*. Mwandishi amewasari kama Makahaba waliolenga kuridhisha utashi miili yao kiashki sio kutegemea pesa. Inadhihirka kwamba uozo wa maadili katika taasisi hii ya kielimu ulikuwa umepita kiasi kwamba usiku wa manane wavulana waliingia malazi ya wasichana na kuwaburura nje kimakusudi na vitendo kama hivi hudhihirisha ukahaba *(Uk 33):*

*…wavulana wakubwa wenye ukware wa Mbwa koko. Na walikuwa mawindo rahisi. Nyakati za kudurusu madarasani usiku zilikuwa na viroja na vioja. Wavulana hao wakiwatoa wasichana mmoja mmoja na kuwaburura nje kama kondoo wanaopelekwa machinjioni.Wafanyaje wasichana wa watu dhalili pale walipo?Almasi alishangaa usiku mmoja alipofumania mvulana mmoja akihema na msichana akilia karibu na safu ya vyoo. Siku nyingi baadaye Almasi alizoea kushuhudia visa kama hivyo.*

Dondoo hili linaakisi kiasi cha ukahaba katika taasisi ya kielimu na kuwa kuna uwezekano wa uozo wa tabia wa aina hii kuambukizwa hata kwa wale wanafunzi wapya wanaojiunga na shule ingawa walitunzwa vizuri na wazazi wao tokea utotoni.

**Nakhumicha**

Mwandishi KenWalibora amemsawiri Nakhumicha kama mhuskika kahaba kwa sababu ni hawara yaani anapata mimba nje ya ndoa na kumza mtoto itwayeDina. Nakhumicha ni dada'ake Almasi, binti Mzee Masasi na Paulina. Alipomzaa dina juu ya ukahaba, alipigwa na baba'ake Masasi nusura kufa *(Uk 21):*

*Mama alimwambia kumhusu dada'ake kifungua mimba Nakhumicha. Sasa kaolewa huko Bajoli wilayani Bungoma. Alikumbukia jinsi Nakhumicha alivyopata mimba akiwa bado kwao. Alikuwa miongoni mwa wasichana kabisa pale kwao kijijini kupata mimba nje ya ndoa. Almasi anakumbukia vile baba'ake alivyotema cheche za hasira na kufoka kama swila mwenye sumu kutokana na kile alichokiita "**Umalaya"** wa binti yake uliomtungisha mimba nje ya ndoa.Mzee Masasi alimpa*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

> *nakhumicha kipigo cha kikatili nusura amwue. Mama alipoona mumnasihi mumewe amwache mtoto hakusaidii kitu alijitupa kati na kusema; " Jamani imetosha. Unaniulia mtoto mume wangu, basi niue mimi mwenyewe. Mara mzee Masasi aliamua kuwaadhibu wote mtu na Mama'ake. Mama na binti wakapigwa wakapigika wakawa hawajiwezi, hawajitambui……*

Dondoo hili ninadhihirisha ukahaba na athari zinazompata mhusika Nakhumicha hata na mama'ake akaathiriwa na matokeo ya ukahaba ingawa hakuhusika kitendo. Mwandishi hapa analenga kuelimisha kwamba, Makahaba matendo wafanyayo huenda huwaathiri wale katika jamii kwa namna moja au nyingine.

**Machuma**

Hatimaye, mwandishi anadhihirisha pia ukahaba katika riwaya hii kwa kumsawiri Machuma binti Mangdelina na Daktari Makabila aliyefariki wakati alipokuwa anaharibu au anatoa mimba. Machuma ni mhusika mdogo tatika hadithi hii yya*Ndoto ya Almasi* (Uk 112):

> *Mangdelina mke wa tatu wa Daktari makabila yule aliyekimbia kumwita mumewe aje kumzuia Mzee Masasi kumwangamiza nakhumicha na mama'ake wakati Nakhumicha alipopata himila nje ya ndoa alikuwa na ombi lake pia. Alikuwa muumini mwenzake Paulina binti Nikasio katika madhehebu ya Sanda Rula. Naye Alikuwa akiwa ametokwa na jasho na kuhemahema.Alihofia huenda akafika akiwa amechelewa mno.Akampa barua na kumpa barua Mama Almasi ampelekee binti yake Machuma aliyekatika akiwa bado mbichi katika harakati za za kujaribu kutoa mimba.*

Dondoo hili laonesha msichana Machuma anayeshiriki vitendo vya ukahaba. Hii inathibitisha kwamba kisa hiki ni cha ukahaba kwa sababu ya kupata mimba nje ya ndoa, asingalifulia katika harakati za kutoa mimba, angekuwa anaitwa hawala ambalo ni jina sambamba na ukahaba.

***Mtazamo wa Mwandishi Kuhusu Ukahaba***

Katika kuhakiki Riwaya ya *Ndoto ya Almasi*tumeona kuwa mwandishi KenWalibora amewachora wahusika wake Almasi, Nakhumicha,Chemtai, wanafunzi, Machuma, Mzee Masasi, Chebosio na mama Chebosio. Mwandishi aliwasawiri wahusika wake wkiegemea matazamo wa kiutekelezi unaosisitiza kwamba mwanamke au mwanamume hushiriki ukahaba kwa ajili ya sababu mbili yaani Sababu za kiuchiumi na sababu za kuridhisha miili. Alakini katika usawiri wake, amezingatia kipengere cha kuridhisha miili iliyo na uchu wa mapenzi, haoneshi kisa chochote ambapo mhusika fulani anashiriki ukahaba kwa madhumuni ya kupata pesa au zawadi bali wahusika wake wote wanajitumbukia katika jangwa la ukahaba kwa sababu mmoja imeyotanguliwa hapo juu. Tukiuchukulia kabisa mfano wa wanafunzi wa shule ya upili StJoseph's, mwandishi hapa anaonesha kiasi cha hisia za vijana katika katika jamii, zisizotunzwa na kukosolewa ingalimapema, vijana kama hawa hupata na bahari la matatizo na si wao peke yao bali hata jamii hupata athari hizo hasi. Kwa mfano, mwandishi anamwonyesha mhusika, Nakhumicha anapopata mimba, anapopewa adhabu za micharazo ya viboko kutoka kwa baba'ake, Mamake Paulina alipoingilia katikati ili kumzuia baba akomeshe mapigo kama ya punda, mama naye akapewa makofi kiasi cha kutosha kama vile ndiye aliyefanya kosa.

Hali hivyo, inaelekea kuwa lengo la mwandishi huyu halikuwa hasa kuzionesha kwa undani athari hizo za ukahaba, bali ni kusisitiza masaibu wanayokutana nayo wasichana na wavulana wanaoshiriki mapenzi wakiwa wangali mabichi wa kufanya ndoa. KenWalibora anadhihirisha kwamba mbali na maradhi ya zinaa, ukahaba una adhabu zake za moja kwa moja kwama vile kupigwa lakini iliyo hatari sana ni kupoteza uhai yaani kufa. Tukimwangalia mhusika kwa jina la Machuma baada ya kubebeshwa mimba anaamua kuitoa kama mkakati wa kujiepusha aibu kwa marafiki zake, wazazi na jamii kwa jumla lakini mambo yakamwendea kinyume hatimaye akakaka kamba.

Mwandishi pia anagusia suala la kujikinga hali inayoweza kusababisha shida; twamwona mhusika Almasi anavyomruhusu kutazama bastola yake pale mtoni, naye akamalizia ameangukia mtegoni kwani hisia za mapenzi hazijui sura, rangi au mamlaka, maskini au tajili, mfupi au mrefu, mwerevu au mpumbavu , ni kirusi chenye sifa sawishi, ukishikwa hivi punde utajitambua baada ya mchezo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

wa bila firimbi na ushindi wa magoli kadha wa kadha. Hapo basi, mwandishi ingawa hakuzichora kwa kina athari zinazowapata wahusika, anataja ukahaba kama kitendo hasi.

Kwa ujumla, kulingana na nadharia zimezotumia na mtafiti, nadharia ya utekelezi imefaa uchambuzi wa kazi ya KenWalibora (*Ndoto ya Almasi*) kulingana na vile anavyowasawiri wahusika wake. Nadharia ya utekelezi huzingatia vigezo viwili yaani kigezo cha fedha na kigezo cha kuridhisha nafsi. Mwandishi wa riwaya hii amejikita katika katika kipengere cha kuridhisha miili kama sababu kuu ya kufanya ukahaba bila kuingiza kigezo chochote hata zawadi. Wahusika wake wote wanaonesha udhaifu wa nafsi na hatimaye huishia katika pilikapilika za ukahaba. Kwa mfano, Chemtai baada ya kuiona bastola ya umeme papo kwa hapo akapandwa na miungu ya mapenzi ikamzunguka kama umeme usioua, hali ikachangamka hadi auridhishe mwili wake. Kwa upande wa Almasi, alikuwa kama vile hataki pale mwanzoni, lakini miale ya mapenzi na utashi wa kuridhisha mwili ulipozidi kutetemesha kimemeshi chake akili zikamtoka na kumtembelea jirani na hapo basi mchezo wa primia ya Ulaya ukaaza bila malipo yoyote.

Licha ya hayo yote, mtazamo wa mwandishi Mohamed S. Mohamed wa riwaya ya *Nyota ya Rehema* ni tofouti na ule wa KenWalibora. Mohamed kutokana na vile anavyosawiri wahuka wake, anadhihrisha ya kwamba baadhi ya watu hufanya ukahaba kwa ajili ya kupata pesa au zawadi. Tukiwaangalia wahusika kama vile Ruzuna, Kidawa na chiku, ukahaba ni kazi yao ambayo wanaamnini kwamba wataitegemea wakati wowote kwa kuwapa mahitaji pamoja na kujinufaisha kiuchumi. ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* lakubaliana na nadharia ya umaksi ambayo imetumiwa na mtafiti katika kazi hii, iegemewa sana haswa katika hali ya wahusika kufanya ukahaba kwa ajili ya kupata pesa.

Swali la kwanza liliuliza: Kuna usawiri gani wa ukahaba na wahusika makahaba katika Riwaya za Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi? Kama ambavyo imebainishwa, ukahaba limedhihirishwa katika riwaya hizi. Waandishi wengi wa riwaya, wakiwemo wa Nyoya ya Rehema na yule wa Ndoto ya Almasi wamesawiri baadhi ya wahusika wao wakijihusisha na suala hili. Katika riwaya ya Nyota ya Rehema kwa mfano, mwandishi amewabainisha wahusika kama vile; Rehema, Ruzuna, Chiku, Kidawa na Bwana Mansuri kama wahusika wanaojishirikisha na Ukahaba. Aidha, katika riwaya ya Ndoto ya Almasi mwandishi amewabainisha wahusika kama vile Almasi, Chemtai, Chebosio, Wanafunzi wa shule ya StJoseph’s na Mzee Masasi kama wahusika wanaojihusisha na vitendo vya Ukahaba.

## HITIMISHO

Utafiti huu ulichunguza ukahaba katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni riwaya za *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi*. Lengo kuu ni kuangalia usawiri wa suala hili katika riwaya zilizoteuliwa yaani jinsi waandishi wa kazi hizi za kifasihi wanavyosawiri ukahaba na msimamo wao. Kwa hakika kipengele hiki cha kulinganisha ukahaba katika riwaya hizi mbili, tafiti zilizotangulia zilijikwepa. Utafiti huu umebainisha kuwa usawiri wa ukahaba katika riwaya ya *Nyoya ya Rehema na Ndoto ya Almasi* ni tofauti kulingana na jinsi waandishi walivyolisawiri suala hili kimtazamo. Katika riwaya zote mbili, waandishi wanawachora baadhi ya wahusika wakiwahusisha na vitendo vya ukahaba lakini hawaoneshi kwa kina athari zinazowapata wanajamii na msimamo wa jamii kuhusu suala hili. Katika *Riwaya ya Nyota ya Rehema* mwandishi anamuonesha mhusika Rehema akifanya ukahaba na Bwana Mansuri, Bi Rose alipopata fununu kuwa mumewe anafanya ukahaba na yaya, akaamua kumfukuza nyumbani yaya huyo ambaye ni Rehema. Lakini mwandishi Mohamed Sulaiman Mohamed hatuonyeshi athari zilizoipata ndoa ya Bi Rose na Mansuri hapo baadaye. Vilevile, katika *Riwaya ya Ndoto ya Almasi*, mwandishi anamuonesha mhusika Chemtai akijihusisha na ukahaba kwa kufanya mapenzi na wanaume mbalimbali hata wa kabila tofouti, watoto aliokuwa nao walikuwa wa mababa tofouti lakini haoneshi matatizo yaliyomkabili mhusika huyu Chemtai katika matendo yake ya ukahaba na ikiwa; je! aliendelea kuwatunza watoto hao yeye mwenyewe au aliwatunza na msada kutoka kwa baba zao?, alitarakwa na mke wa pili wa mzee Kirwa au kasamehewa?.

Kwa sababu hiyo, ni wazi kuwa waandishi wa *Riwaya ya Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

hawakufafanuakwa kina ukahaba kwa kudhihirisha athari zote zinazoweza kuwapata hata vijana na wanajamii wengine wanaojishughulisha na utendaji wa ukahaba. Ukosefu wa kufafanua kwa kina ukahaba na athari zote ziliomo, huacha pengo la kutowapa wasomaji mafunzo kamili kuhusu ukahaba maana kwamba wasomaji hawatapata faida hasi na chanya kuhusu kahaba.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulichunguza ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi*. Kwa hakika, hakuna utafiti ambao unaweza kuchukuliwa kuwa umekamilisha suala husika katika mada ya utafiti. Hivyo basi, ni wazi kwamba utafiti huu haukudadavuliwa na kutosheleza ukahaba katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti zaidi unahitajika kuchunguza ukahaba katika kazi nyingine za fasihi kama vile; Ngano, mashairi/ nyimbo, hadithi fupi na tamthilia. Halikadhalika utafiti wa ziada unaweza kufanywa kwa kuzingatia kipengere cha uchambuzi linganishi wa ukahaba katika kazi ya kifasihi yoyote na uhalisia wake katika jamii.

**MAREJELEO**


Bakwesegha, C. (1982). *ProfilesofUrbanProstitution.* A casestudyfrom Uganda. (Kenya Literature Bureau, Nairobi).

Ken. Walobora. (2006), *Ndoto ya Almasi*.(Moran EastAfricapublishers Limited

Kezilahabi, E. (1971). *RosaMistika*. (East African Literature Bureau).

Kishtainy, K. (1982), *The ProstituteinProgressiveAliterature.* AlalinsonandBusby Ltd:

Kothari, C. R (2004) *ResearchMethodology: MethodsandTechniques.* New Age International (P). New Delhi India.

Lowry, R.P. (1974), *SocialProblems*: A CriticalAnalysisofTheoriesandPublicPolicy.

Mwandishi wa Kike na wa Kiume Uchunguzi Katika Riwaya Teule". Tasnifu ya M. A. Kiswahili .Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Madumulla, J. S. (1987). *"Maendeleo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania",* ktk: Kiswahili . Dar es Salaam:TUKI.

Mbah,F.U (1979) *Ukahaba katika Tanzania Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar es salaam*

Mbilinyi, M. (1983), *Mwanamke wa Tanzania:*AnalyticalBibliography. (MotalaCrafisika, Sweden).

Mlacha, S.A.K. (1984), "*Riwaya za Visiwani* (1970-1980) na Ujenzi wa Jamii Mpya", katika *Mualika*. Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S.A.K. (1993), *Kiswahili NovelsandSociety*.Dar es Salaam University Press.

Mohamed, M.S. (1972), KIU. (East African Publishing House). (1976). *Nyota ya Rehema*. (OxfDrd University Press).

Mohamed, S.A. (1977), *Asali Chungu*. (Shungwaya Publishers Limited, Nairobi). 132

Muga, E. (1980), StudiesinProstitution: East, West and South Africa, Zaire andNaveda. Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Nguma, N. (2001), Taswira ya Mwanamke Jinsi Ilivyochorwa Katika Riwaya ya Kezilahabi. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Saumu Juma Khamis (2017), katika utafiti wake; *Kuchunguza ukahaba katika riwaya ya Kiswahili* ; mifano katika *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi*.

Senkoro, F.E. M.K. (1982), *Ukahaba katika fasihi ya Kiafrika.* (Tanzania Publishing House, Dar es Salaam).

Shafi, S. A. (1999), *Vuta N'kuvute.* Dar es Salaam. Oxford University Press.

Smart, C. (1976), *Women, CrimeandCriminology.* (RoutledgeandKegan Paul).

Strobel, M.N. (1975), *Mwanamke mwislamu mjini Mombasa, Kenya 1966-1973.* (Tasnifu ya

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1005

Ph.D., Chuo Kikuu Cha California, Los Angeles).

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press